# NGURUMO ya MWANDISHI

Toleo La IX-Juni-MMXXII





## Jivunie vya nyumbani, Muunge fanani

*Toleo maalum la Elite Mjue Mtunzi²*

02 Dawati la Mhariri: 0766-974 865

# JIVUNIE VYA NYUMBANI, MUUNGE FANANI

*Jivunie vya nyumbani… Muunge fanani!*

Hii ndiyo salamu tuliyofundishwa huko kwenye hafla ya Mjue Mtunzi msimu wa pili. Asante kwa wote waliofikiri juu ya hili jambo.

Leo katika tahariri yangu napenda kuzungumza kuhusu mambo haya mawili; la kwanza …'Vya nyumbani' na la pili 'muunge fanani'.
Nchi yetu ni moja kati ya nchi zilizokaliwa na wakoloni kwa muda mrefu sana kabla ya kupata uhuru. Nchi yoyote inayokaliwa na wakoloni huachwa na athari za kikolonikoloni kwa sababu, mkoloni hata akiondoka huwa anapenda kuuacha ukoloni wake kichwani mwako.

Nini maana ya ukoloni? Kila mtu ana jibu lake. Lakini la kwangu mimi ni hili: Ukoloni ni hali ya mtu kumtawala mwingine bila matakwa yake. Ili mtu akutawale kwanza anatakiwa kukuvuruga akili yako na kufanya yeye aonekane bora kwako na wewe ujidharau mwenyewe.

Amini usiamini, kama wazee wetu wa zamani walioishi huko Isimila, Engaruka, Olduvai na kwingineko wangeendelea na maisha yao ya asili, basi Afrika yetu ingekuwa mbali sana. Waliwinda kwa mikuki ya mawe iliyowekwa mpini wa mti, walichinja wanyama kwa visu vilivyochongwa kwa mawe, waliunda mashoka, viwembe kwa mawe hayohayo. Wakishachuna mnyama basi ngozi ileile waliitumia kujisitiri.

Ikawa asubuhi ikawa jioni, wakafika watu wengine kutoka upande mwingine wa dunia ambao walileta kila kitu. Kitendo cha kuingiza zana zao walizoziita za kisasa kikawafanya wazee wetu wabweteke. Vile walivyovumbua wao na ambavyo bado vilikuwa vikiendelea kuboreshwa wakaviona havina maana. Wakaviweka kando na kutumia vya kigeni. Hapa ndipo tulipoanza kutawaliwa.

Mtu yeyote anayekung'ang'aniza utumie chake kwa kuwa ni bora na ukakubali huo ndiyo ukoloni. *Anyway,* sitaki kufundisha historia isiyikuwepo kwenye mtaala.

Ninachotaka kusema ni kuwa kujivunia vya nyumbani ndiyo uzalendo wenyewe. Sijasema tuchukie vya wageni la hasha! Bali vyetu hatuna budi kuvitukuza kwanza.

Siku moja nilikuwa na msomaji mzuri wa vitabu, nikamuuliza swali, vitabu vipi anapenda kusoma, akanijibu 'vya riwaya lakini siyo vya Kiswahili…' nikapata ukakasi kidogo. *Anyway,* kila mwisho wa mwaka watu wengi hupenda kutoa orodha ya vitabu walivyosoma kwa mwaka, lakini utashangaa vya Kizungu asilimia 85 na vya kikwetu asilimia zilizobaki.

'Hakuna waandishi Tanzania!' nani alikwambia? Wanafalsafa wa Kitanzania wanasema 'mkataa kwao mtumwa'. Ni kweli, kama hujivunii vya nyumbani, unajivunia vya wageni tu, tukuweke kundi gani? Mtumwa.

Penda vya nyumbani ili umuunge fanani.
Jambo la pili mi 'Muunge fanani'. Fanani ni yule anayekuletea simulizi kwenye kitabu. Kwa kupena vya nyumbani basi asilimia kubwa utakuwa umemuunga mkono fanani. Kwa kununua kitabu cha nyumbani utakuwa umempa moyo mwandishi. Tanzania ina vipaji vikubwa vya uandishi, lakini vitaonekana vipi kama wewe msomaji unasoma vya '*wasosorino'* unaacha vya nyumbani? Hebu tubadilike… Tamasha la Mjue Mtunzi msimu wa pili limetutaka wasomaji kubadilika. Si kwamba tusisome vya Ughaibuni, la! Bali nguvu nyingi tutumie kuwaunga mkono waandishi wa ndani.

Mwisho niwapongezxe sana UWARIDI chini ya Rais Hussein Issa Tuwa kwa kufanikisha kila lililokuwa jema. Naamini kinachorudi ni kikubwa kuliko kinachokwenda.

Amin.
***Richard Mwambe, 15 Juni2022***

**<u>NGURUMO YA MWANDISHI</u>**

**MHARIRI: RICHARD MWAMBE**

**MSAIDIZI: REY STANLEY**

**<u>WASILIANA NASI</u>**

**0766 974 865 AU 0672 160 016**

# 03 MJUE MTUNZI ILIVYOLISIMAMISHA JIJI

**Na Mwandishi wetu**

TAMASHA kubwa la waandishi kwa wasomaji wa vitabu hususan vya riwaya lililojulikana kama Elite Mjue Mtunzi msimu wa pili limetikisa Jiji la Dar es salaam na vitongoji vyake.

Tamasha hilo lililofanyika katika ukumbi wa NSSF Ilala lilihudhuriwa na wapenzi wasomaji wa riwaya zaidi ya mia mbili kutoka ndani na nje ya jiji hilo.

Kauli mbiu ya siku hiyo 'Jivunie vya nyumbani, muunge fanani' ilibeba umaana mzima wa jina la tamasha. Katibu Mwenezi wa Umoja wa Waandishi wa Riwaya wenye Dira 'UWARIDI' Ndugu Maundu Mwingizi alisema, 'Sisi kama watunzi ndiyo tunaoweza kumuelezea mtunzi'.

Kwa kuwa tamasha hilo liliwakusanya pia wasomaji, Katibu Mwenezi wa umoja huo Ndugu Maundu alienda mbali zaidi na kufafanua uhusiano unaokuwapo kati ya mwandishi na msomaji kwa kumuelezea msomaji kama mdadisi wa kiakili wakati udadisi huo wa akili ndiyo kazi inayofanywa na mwandishi wa riwaya.

Aidha aliyekuwa mgeni rasmi katika tamasha hilo Waziri wa Elimu Mheshimiwa Adolf Mkenda (MB), katika hotuba yake alisema wazi kuwa Serikali itaunga mkono kwa kufadhili matamasha hayo ili kuongeza hamasa kwa washiriki wengi zaidi.

Naye mwakilishi wa Mdhamini wa tamasha hilo kutoka Elite Book Store, Damian Hemes alisema kampuni yake itaendelea kufadhili tamasha hilo kwa kuwa kupitia usomaji wa vitabu, watu wanapata historia ya nchi kwani maandishi yanabaki vizazi na vizazi.

Tamasha hilo lilihudhuriwa pia na Mwandishi nguli Shafi Adam Shafi, Profesa Joseph Mbele, Profesa Penina Mrama, Profesa Emmanuel Mbogo, Dokta Felista Mahonge na wanazuoni wengine wengi waliolipa uzito tukio hilo.

Katika tamasha hilo pia kulitolewa ngao maalum kwa waanidishi watatu. Ngao hii inayojulikana kama Ngao ya Mtunzi ilitunukiwa kwa mwandishi na Mshairi Ibrahim Gama, Mwandishi na mwanahabari wa magazeti ya Global Publishers Joseph Shaluwa na Mwandishi na Mwanahabari wa TBC Elizabeth Mramba.

Licha ya ngao hizo, katika tukio hilo pia kumezinduliwa vitabu vya waandishi mbalimbali, tukio ambalo liliufanya ukumbi huo kuzizima.

Tamasha la Mjue Mtunzi msimu wa pili, lililodhaminiwa na Elite Book Store liimeacha alama kubwa katika tasnia ya uandishi wa riwaya nchini. Hatuna budi kuwashukuru wote walioandaa kwa hali na mali.
*Jivunie vya nyumbani…..*




**Penda kusoma vitabu**

www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

**Faida za kusoma vitabu:**

> Msisimko wa Akili

> Kupunguza Msongo wa Mawazo

> Kuongeza Ujuzi wa mambo mbalimbali

> Kuongeza Msamiati

> Huboresha Uwezo wa Kukumbuka

> Hukupa Uwezo Mkubwa wa kuchambua na kufikiri

> Huboresha Mtazamo na Umakini

# 04 ALILOSEMA HUSSEIN ISSA TUWA RAIS WA UWARIDI BAADA YA ELITE MJUE MTUNZI

**Na. Richard Mwambe**

**Hili ndilo alilolisema Rais wa UWARIDI baada ya tukio. Simu kutoka Ngurumo ikaunguruma kiganjani mwake. Ngurumo ya Mwandishi ikamtaka aseme mambo mawili tu kama ifuatavyo:-**

Unalizungumziaje tukio la Elite Mjue Mtunzi season 2 kwa ujumla wake?

Tukio la Mjue Mtunzi, Elite Mjue Mtunzi, naweza kusema kuwa ni tukio lenye mafanikio makubwa sana. Nasema hivyo kwa sababu waliohudhuria lile tukio watakuwa mashahidi kwamba tukio limekuwa bora, kulikuwa na zinduzi za vitabu sita, tumepata mgeni rasmi  kutoka serikalini, Waziri wa elimu Prof. Adolf Mkenda.

Vilevile tumetoa ngao tatu kama ilivyokuwa msimu wa kwanza. Ngao hizi zimekuwa bora zaidi ya zile za kwanza japo thamani yake ni ileile. Pia tumefanya katika ukumbi ulio bora zaidi kuliko ule wa mara ya kwanza.

Lakini kikubwa zaidi katika Elite Mjue Mtunzi msimu wa pili, tumepata udhamini mkubwa kutoka Elite Bookstore. Huu ndiyo upekee unaoonekana katika Elite Mjue Mtunzi Msimu wa pili.

Msimu wa kwanza tulipata shida sana kupata wadhamini, kupata watu wa kutuelewa tunataka nini, hatukupata *suppor*t lakini safari hii tumeeleweka ni kwamba tumefanya kazi kubwa ya kuelewesha jamii pana ya wadhamini na wafanyabiashara mbalimbali, na hatimaye tumefanikiwa kupata ule udhamini wa Elite Bookstore.

Kwahiyo nalizungumzia kwa ujumla wake ni tukio lenye mafanikio makubwa zaidi, lenye ukubwa zaidi, lenye mwonekano  bora zaidi na lenye thamani kubwa zaidi. Asante!

Unawaambia nini wapenzi wa vitabu kwa tukio lijalo?

Sasa kuhusu wapenzi wa vitabu kwa tukio lijalo. Kwa tukio lijalo ninalowaambia ni kwamba kwanza wakati tunaliendea tukio lijalo, wapenzi wa vitabu nawashauri wazingatie sana kuifanyia kazi kaulimbiu tuliyokuja nayo msimu huu wa pili ambayo inasema 'thamini vya nyumbani muunge fanani'. Kaulimbiu hii inawasisitiza wasomaji kununua kazi za nyumbani zinazoandikwa kwa Kiswahili na miongoni mwao tupo waandishi wa UWARIDI na wengine pia. Wasibague wanunue tu kazi, yaani watu wajenge utamaduni wa kununua vitabu ili sasa tunapofikia kwenye Mjue Mtunzi ijayo tuwe tumeshavuka hii hatua. Tuje na kaulimbiu nyingine kutekeleza jambo jingine, kwa sababu waandishi tunajitahidi sana kuandika, na wasomaji wanafanya kila waliwezalo kununua lakini waongeze kasi kwa sababu sisi waandishi tumeshaongeza kasi ya kuandika. Hasa ukizingatia serikali kupitia Waziri Mkenda pale kwenye Elite Mjue Mtunzi ilitangaza sasa kuja na tuzo mahususi ambazo zitakuwa zinaratibiwa na serikali yenyewe za waandishi wabunifu.

Sasa hii peke yake ni chachu kwa sisi waandishi lakini je; wasomaji wamejiandaa vipi kupokea changamoto hii ya vitabu kuja kwa wingi kutoka kwa waandishi.

Kwa hiyo mimi ninavowaambia , tunavyoelekea kwenye tukio lijalo, watuoneshe sasa katika kipindi hiki cha mpito kutoka hapa, baina ya sasa na tukio lijalo kwamba wao wapo pamoja na sisi katika kutuunga mafanani, kuonesha kwamba wananunua kazi zetu.

Na kutuunga wasichukulie kama vile kutuunga wanatusaidia! Hapana! Yaani kutuunga ni kama kututuza, kutufanya tuendelee kuandika. Kwa sababu tukiona kazi zetu zinathaminiwa kwa kununuliwa, tutaendelea kuandika. Hilo moja.

Lakini la pili; kuelekea kwenye tukio lijalo, wategemee makubwa zaidi, wategemee mashtukizo zaidi, nikisema mashtukizo ina maana *surprise*. Wategemee mashtukizo zaidi, kwa sababu upande wetu kama waandaaji wa hili tukio, tuna vitu vingi sana  vinavyohusiana na vitabu ambavyo tuna taaluma navyo, tuna ujuzi navyo, na tuna uzoefu navyo na tuna maono navyo ambavyo tusingekuwa na jukwaa hili tusingepata pa kuvionesha. *So far*, tumeonesha vitu kwa awamu awamu. Tukio kimsingi linakuwa kama saa nne tu, halina muda mrefu. Kwa hiyo hatuwezi tukatoa vitu vyetu vyote katika tukio moja. Kwa hiyo watarajie mapya, makubwa, mazuri, mashtukizo zaidi katika Mjue Mtunzi Ijayo. Asante.

# 05 UZINDUZI WA VITABU: 'CHAWA' CHAMLETA MOLITO KIVINGINE

**Katika vitabu vilivyozinduliwa katika tamasha la Elite Mjue Mtunzi msimu wa pili, CHAWA kilikuwa kimojawapo kilichouteka ukumbi.**

**Hapa mwandishi Hussein Molito anatuambia machache kukihusu.**

Chawa ni hadithi inayomhusu Bukindo Masumbuko. Mwanafunzi bora mara mbili chuoni IFM. Shahada ya kwanza akipata GPA ya 4.6 na Shahada ya Uzamili akipata GPA ya 4.8. Licha ya vyeti vyote hivyo kutafsiri kufanikiwa kwa kiwango cha juu kwenye masomo yake, havikufanikisha kumpatia kazi kwa takribani miaka minne. Maisha magumu yakamfanya aghushi cheti cha usafi, angalau ajaribu bahati yake. Maana kwa wakati huo alihitaji kazi yoyote tu ilimradi mkono uende kinywani.

Cheti kilichotengenezwa ndani ya nusu saa kwa gharama ya shilingi elfu 5, ndicho kilichompatia ajira ndani ya wiki moja pekee. Pesa huja na starehe na matatizo ndani yake. Ni kipi kilichomkuta kijana huyu baada ya kubobea kwenye kazi yake hiyo isiyo halali? Akiwa kama mmoja wa wafanya usafi kwenye kampuni ya Mr. Kizito, anagundua fursa nyingine nje ya kazi hiyo nje yenye mshahara mdogo. Fursa iliyomfanya apate mafanikio makubwa kwa muda mfupi.

Fursa ambayo ilimfanya awe anatabasamu usoni ila moyo wake unaungua. Hali ya kuitikia 'ndiyo' kwa kila kitu anachotumwa ili hali kuna muda nafsi yake inakataa. Ikaanza kumtesa japo ilimuinua kiuchumi.

Bukindo aliitafuta nafasi ya kuwa CHAWA wa bosi wake kwa udi na uvumba, akafanikiwa kuipata. Msomi mwenye shahada ya uzamili, akawa kuwadi. Ujira wake akaupata baada ya kuuza wanawake kwa bosi huyo asiyejali utu wala heshima yake. Ungana na Bukindo Masumbuko kwenye kibaraka wa Bosi. Ana mengi ya kuburudisha na kutufundisha.

Wazo la kuanika CHAWA lilikujaje?

Kwanza kabisa hili wazo lilikuja kimasihara sana. Nilikuwa nyumbani kwa mama, nikamsikia Baba Levo akimsifia Bosi wake Diamond Platnumz na kufika mbali kuwa yu tayari kumzalia mtoto. Hapo ndo nikajiuliza kwanini amehiyari kujidhalilisha, nikagundua anafanya hayo ilimradi tu watu wamwongelee yeye na bosi wake. Nikapata wazo niandike kuhusu hawa wapambe, ila kwa sababu tofauti. Ndipo likaja wazo la Kuandika Kibaraka wa bosi ambaye amepata kazi baada ya kufoji cheti cha *Cleaning.*

Wazo la kumtengeneza chawa mwenye shahada ya Uzamili tena kwenye mfumo wa Ukuwadi ndo ladha ya hadithi hii ilipo. Na ni moja ya hadithi nilizoandika kwa muda mfupi sana. Licha ya kuwa sikuandaa "Hints" pembeni kama nifanyavyo kwa hadithi nyingi, sikupata "Writers Block" hata mara moja. Ni hadithi niliyoiandika kibosi pia, maana mara kadhaa nilikuwa na kinywaji changu pendwa pembeni. Nimechapa vitabu Tisa kabla ya kutimiza hiki kuwa kitabu cha kumi chenye mapinduzi ya ajabu. Kwanza ndo kitabu nilichochapa nakala nyingi zaidi.

Nimechapa nakala 1500. Kwa mara ya kwanza nimefanikiwa kukizindua baada ya kupata bahati kwenye Tamasha la Mjue Mtunzi. Tukijaaliwa uhai, tarehe 7 ya mwezi wa 8 nitafanya sherehe ya utiaji sahihi wa kitabu hiki na kila kitabu changu ambacho msomaji amekinunua. Tutafurahi na kupata mziki laini kutoka "live band" Kitabu kinauzwa shilingi elfu 10 pekee. kinapatikana kwenye maduka yote ya Elite bookstore, Creative Ideas Kariakoo, Kona ya Riwaya Kinondoni block 41 na Posta pale kwenye askari, muuza magazeti anaitwa George.



06

# MBONECHE ATULETEA 'WARAKA'

**Elite Mjue Mtuzi msimu wa pili hakika ilitufanya tuwajue watunzi. Huyu hapa Hassan Mboneche, naye alizindua 'WARAKA' anasema…**

Julai 3, 2022 imekuwa siku yenye furaha maishani mwangu. Siku ambayo haitoisha kuikumbuka, na ni siku itakayonifanya nijivunie wakati wote. Kupata wasaa wa kuzindua kitabu changu cha riwaya ya WARAKA katika tamasha la Elite Mjue Mtunzi msimu wa pili, ndiyo inayonifanya nizungumze yote haya, kutokana na ukubwa wa tamasha, pamoja na ugeni uliohudhuria.

Kitabu hiki ni kimoja, miongoni mwa vitabu saba vilivyozinduliwa na mgeni rasmi, Mhe. Prof. Adolf Mkenda, Waziri wa Eimu, Sayansi na Teknolojia mbele ya wadau mbalimbali wa kazi za kisanaa. Ni fahari iliyoje, na heshima ya kipekee, kwani historia haifutiki. Waraka ni riwaya inayoelezea madhila mbalimbali yawakumbayo watu wema wanaovaa ujasiri wa kufichua maovu. Hasa wafichuliwao wakiwa kwenye nyadhifa. Ijapokuwa sio wenye nyadhifa tu nd'o hawapendi kufichuliwa maovu yao, bali mwanadamu kwa asili ameumbwa kwa hulka hiyo. Watu wengi, waliojaa hali hii hujitahidi kuuchukulia uovu kama dhahabu kwa sababu hawataki jamii ifahamu.

Hilo limejidhihirisha katika riwaya hii inayosadifu tawala za mataifa kadhaa hapa duniani. Hilo limedhihirishwa humu kupitia kwa Waziri wa Ulinzi wa nchi ya Tuleane akishirikiana na vibaraka wake viongozi wa ngazi za juu wa jeshi la ulinzi. Ambapo kwa ujumla wanajitahidi kuzififisha jitihada za rais kufikia azmaye. Chanzo cha haya, ni kufuatia kifo tatanishi cha aliyekuwa Waziri Mkuu wa nchi hiyo na kutekwa kwa rafiki yake kipenzi siku chache baada ya kifo chake.

Nchi ikaingia katika tanziko na shauku ya kufahamu sababu, ndipo anapojitokeza rais kupigilia msumari wa hatua hizo. Kwamba lazima chanzo kifahamike. Pindi vyombo vya ulinzi na usalama vikifanya bidii ya kutafuta chanzo, anajitokeza mtoto wa marehemu Waziri Mkuu na kutoa ahadi ya kuzungumza na umma kupitia vyombo vya habari avisaidie vyombo vya ulinzi vilivyopo majukumuni kuwaeleza wahusika wa matukio hayo kupitia waraka ulioachwa na babaye kabla hajakumbwa na mauti. Maamuzi ya binti huyu pindi wananchi wakiyapokea kwa furaha kwamba wanaenda kukata shauku yao ya muda mrefu, mambo yalibadilika ghafla na hatimaye kuongeza matatizo tofauti na ilivyotarajiwa hapo awali. Hapa ndipo zilipojionesha rangi halisi za mwanadamu.

Kwani ilizaliwa vita ya vuta n'kuvute kwa kila upande kuutaka waraka huo kabla haujawa wimbo masikioni mwa wengi. Kwa ufahamu wa mengi yaliyomo, kwa utambuzi wa nani ambaye alifanikiwa, na kilichobebwa ndani ya waraka huo, wadau wanaweza kununua nakala ya kitabu hiki kwa gharama ya TZS 10,000/= watapata unono wote taratibu na kwa utulivu mkubwa. Hii ni kazi niliyoiandika kwa mara ya kwanza mnamo mwaka 2019, na nilibahatika kuweka baadhi ya machapisho yake katika kuta zangu za mitandao ya kijamii, lakini sikuhitaji iishie huko, ndipo nilipodhamiria kwa dhati kuwafikia walaji katika mfumo wa nakala ngumu.

Na nimefanikiwa. Kitabu hiki ni bora, na nimejali afya ya macho ya watu kwa asilimia mia moja. Hivyo niwatoe hofu kwa wale wenye matatizo hayo. Watasoma kitabu hiki kwa uzuri na amani huku mioyo ikitakasika. Mwisho, napenda niwafahamishe kwamba kitabu hiki kinapatikana jijini Dar es salaam pekee kwa sasa, katika maduka ya Elite Bookstore, Kona ya Riwaya-Kinondoni na Creative Ideas-Kariakoo. Lakini kwa siku za baadaye kitapatikana kwa mawakala mbalimbali wa mikoani. Sasa ni wakati wa kujivunia kama isemavyo kauli mbiu ya tamasha hili mwaka huu, jivunie vya nyumbani, muunge fanani.



**Hassan Mboneche, mwandishi wa WARAKA**

# 07 DAVID SHALALI AJA NA 'SALOME WA SADAKA'

**Wakati tumetulia kwenye Elite Mjue Mtunzi msimu wa pili tukiendelea kusimuliwa kwa kifupi vionjo vya vitabu vinavyozinduliwa, ghafla tukaletewa SALOME WA SADAKA. Mwandishi anatusimulia.**

Salome wa Sadaka ni hadithi ambayo niliiandika kama burudani na funzo kwa jamii. Nakumbuka niliiandika tangu mwaka 2017 na kuimaliza mwaka 2018. Ni hadithi ambayo kabla ya kuandika niliwaza sana nikiwa kama mwandishi mchanga ambaye tayari nimewasoma waandishi wakubwa. Nikawa najiuliza nitaandika hadithi gani ili niwe tofauti na wao.
Sasa mimi nikawa na ile hali ya nitoke vipi. Ndipo nikaja na kisa na mtindo ambao ukikipata kitabu hiki, HAKIKA UTASISIMKA UKINISOMA. Hadithi hii inamzungumzia msichana mdogo anayeitwa Salome. Na ipo hivi; Saa nne usiku, akiwa anaingia chumbani kwake kwa matayarisho ya kulala, Salome anakutana na madhila ya ajabu kuwahi kumtokea katika maisha yake. Anabakwa kwa njia ya kustaajabisha. Njia ambayo ni ngumu kumuelezea mtu akamuelewa. Kila mtu anayejaribu kumueleza tukio lililomtokea, anashindwa kumuelewa na kumuona kama ni mtu anayeanza kuchanganyikiwa.
Tumaini pekee linakuwa ni mjomba'ake, anamueleza ukweli ya kuwa, kila siku kuna mtu anakuja nyumbani kwake kumbaka na kisha kutoweka. Mjomba anakata shauri kuja nyumbani kwa Salome ili ajue mbivu na mbichi, Anafika, analala lakini asubuhi kunapopambazuka, Salome anabaini mjomba katoweka katika mazingira ya kutatanisha. Alilala ndani milango ikiwa imefungwa lakini asubuhi mjomba hayupo na milango iko vilevile kama awali. Akabaki njia panda asijue ni nini kilichopo nyuma ya maisha yake. Katika harakati za kuhangaika kutafuta tiba ya tatizo sugu la kubakwa kila siku na mtu asiyejulikana, ndipo inapokuja kubainika kuwa, Salome anaishi na mtu asiyeonekana kwa macho.
Ni nani huyo mtu na kwanini haonekani? Hilo ndo' swali kuu utakalokuwa ukipambana na kurasa kuweza kumbaini huyo mtu.

Hadithi hii itakugusa katika nyanja zote, utacheka, utaburudika lakini pia utahuzunika, mwishowe utaondoka na funzo kubwa katika maisha. Na nakuambia kwa yaliyomo humu yamefanyiwa tafiti za kutosha hayakuandikwa jujuu. Na kuna siri kubwa katika umaliziaji wa hii hadithi.
Na Siri yenyewe ni kwamba hadithi hii nilibadirisha kama mara mbili hivi namna ya kuimaliza ili kumsaidia mtu aliyenipigia simu akidai baadhi ya mambo niliyoandika kwenye hadithi hii hata yeye huwa yanamtokea. Hivyo akawa anaomba nimsaidie. Unajua ilikuwaje? Mwanzoni wakati nimemaliza kuiandika hadithi hii nikawa nairusha mitandaoni baadhi ya vipande vya mwanzo mwanzo Ili watu waisome.
Sasa wakati hadithi inaendelea nikapigiwa simu na mtu nisiyemfahamu. Ni msichana akaniuliza wewe ndiye mwandishi uliyeandika hadithi inaitwa Salome? Nikamjibu ndiyo akaniuliza hicho kisa umekitoa wapi nikamwambia Mimi ni mtunzi wa hadithi mbalimbali lilinijia wazo nikalifanyia kazi kwani kunanini?
Kwa masikitiko yule msichana *(jina nalihifadhi)* akaniambia mambo ninayoandika ya Salome kubakwa na mtu asiyeonekana hata yeye huko aliko yanamtokea. Mh! Nilishangaa kwakweli. Akaenda mbele zaidi na kudai lazima mimi namjua muhusika au mimi ndiye ninayekwenda kumbaka kimiujiza. Nilichoka Kwa kweli. Ikabidi nimueleze vizuri utunzi ni nini na visa huwa tunaviundaje hadi hadithi kukamilika. Hivyo kwakuwa mimi ni mtunzi tu ninayebuni visa ikabidi niimalize kimtindo huu kama nilivyoimaliza kwenye kitabu ili na yeye huko aliko afuate vile nilivyoandika mimi pengine itamsaidia.
Ni kweli aliahidi kukifuata kitabu mara tu kitakapotoka. Hivyo Mimi kama mtunzi nimeitunga hadithi hii nikiwa na malengo mawili; moja kufundisha jamii kwa mambo niliyoandika lakini pili kumuonesha njia msomaji ambaye masaibu ya muhusika katika kitabu naye huwa yanamkuta.

Na majibu yote yapo katika kitabu.




# 08 Baada ya Sarafu ya Gavana na Kifurushi Ikulu, sasa ni KABRASHA LA RAIS

**Huyu ni Yule aliyeandika SARAFU YA GAVANA na KIFURUSHI IKULU. Katika Elite Mjue Mtunzi msimu wa pili katuletea kigongo kipya, KABRASHA LA RAIS.**

**Yeye amebobea kwenye ujasusi… hapa anatusimulia kiduchu kuhusu kitabu hili kilichozinduliwa na Waziri wa Elimu Mheshimiwa Profesa Mkenda. Wilbard Makene anatusimulia…**

Rais Kassim Mabrouk wa Tanzania aliyeingia kwenye mgogoro mkubwa na baadhi ya wajumbe wa chama chake, Chama Mahalia (CM).

Genge la matajiri ndani ya chama lilipanga mbinu chafu dhidi yake. Kwa njia za siri, Rais aligundua mipango yote, anatengeneza kabrasha na kumkabidhi Tamim, mtu wake wa karibu katika duru za usalama. Genge









Lilijua kuwa kabrasha hilo lipo kwa Tamim.

Ndipo patishika nguo kuchanika lilipoibuka. Tamim alipambana kulilinda kabrasha linalowindwa na genge hilo kwa hali na mali. Damu ilimwagika, wenye hatia na wasio na hatia wakapukutika.

Kabrasha La Rais ni riwaya yenye kusisimua iliyosheheni visa na mikasa; visasi, mapenzi, uzalendo na usaliti.

Kwanini Kabrasha La Rais?

Baada ya kuwa nimesoma vitabu vingi, nilipatwa na hali fulani ya huzuni kwa yale wanaowakuta wafanya maamuzi katika hali tata za kiuongozi. Wanatishiwa na magenge yenye kuweka mbele maslahi yao kwa kubinya maslahi ya umma. Magenge yenye kukwapua keki ya taifa na kuigawana wao bila huruma yalinitia simanzi kuu.

Hiki ndiyo Kabrasha la Rais, kamata nakala yako katika maduka yote ya Elite Mjue Mtunzi na Kona ya Riwaya Kinondoni bila kusahau reative Idea Kariakoo.

# 09 ‘KWAHERI’ RIWAYA ILIYOFUMWA KITAALAMU NA HASSAN ALLY HASSAN

**Mambo yalikuwa motomoto siku hii. Mwandishi kutoka Arusha Hassan Ally Hassan naye aliwasilisha kitabu chake cha KWAHERI. Kitabu kilichoandikwa kiufundi kabisa, ambapo ukikisoma tu utajua mwandishi ni mtu wa namna gani. Kitabu hiki pia kilizinduliwa siku hiyo.**

**Hapa anatupatia dondoo fupi kuhusu yaliyomo humo”-**

Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania *(Kazi iendelee).*

Kwa jina naitwa Hassan A. Hassani. Ni mzaliwa wa Manispaa ya Lindi. Kitaaluma ni mwalimu. Kwa sasa ninahudumu nafasi ya Afisa Elimu Vifaa na Takwimu wa Idara ya Elimu Msingi katika Halmashauri ya Jiji la Arusha.

Ni mwandishi wa riwaya za Kiswahili pamoja na vitabu vya usimamizi wa Elimu ya Msingi.
Vitabu nilivyoandika na kukamilika ni viwili ambavyo ni KWAHERI *(Riwaya)* pamoja na kitabu cha usimamizi wa elimu kiitwacho SIRI YA MAFANIKIO YA MAENDELEO YA
ELIMU YA MSINGI KATIKA JIJI LA ARUSHA.

Vilevile, nimeshiriki katika utafiti, uandishi, uhariri pamoja na usanifu wa jalada na kurasa za jarida la Halmashauri ya Jiji la Arusha linaloitwa – FAHARI YA JIJI LA ARUSHA.

Kwa uchache sana naomba uniruhusu niielezee riwaya yetu ya KWAHERI.

Riwaya ya Kwaheri inahusu nini?

Ni riwaya inayosawili nchi ya Tanzania ikielezea mapito ya kiutawala na masuala ya kijamii yanayoibuka na kuleta tafakuri kwa wanajamii kuhusiana na utamaduni;
matakwa ya vijana yanayogongana na yale ya wazee na matarajio ya jamii; Suala la utaifa na matatizo yake. Pia kimesheheni masuala la elimu, sayansi, siasa, jografia na utalii, tiba, uzalendo, umaskini, magonjwa, mapenzi na ndoa, rushwa, uongozi mbaya, umuhimu wa elimu, ufujaji wa mali za umma.

Kwa kiasi kikubwa, maudhui yaliyomo katika kitabu hiki yanazihusu nchi nyingi zinazoendelea.

Yapi yanaifanya Riwaya ya Kwaheri kuwa cha kipekee?

Kwaheri ina viwango vingi vya usawiri ambavyo vinakwenda sambamba na kuingiliana pale inapobidi katika masimulizi yaliyofumwa vyema visa na mikasa inayochokonoa mahaba, urafiki, masaibu, jiografia, utaifa, elimu, siasa, tiba, TEHAMA na maarifa ya kitaalamu yatokanayo na tafiti.

Lugha iliyotumika ni sanifu lakini ya kisasa; lugha ya vijana, ya mitaani, darasani, michezoni, mapenzini – ambayo msamiati wake unaongeza utajiri katika hazina ya maneno ya Kiswahili. Uwepo wa matumizi ya nukuu za viongozi wa Kitaifa mathalani Mhe. J.K Nyerere, Mhe. Edward Sokoine, Benjamin Mkapa, Dkt. John Pombe Magufuli, Pia nukuu za
Wanafalsa, Wanasaikolojia pamoja na Wanaharakati kama vile Plato, Alfred Banet, Hilgard, William Ellery Channing n.k, zimetumika katika kufikisha ujumbe uliokusudiwa.

Nyimbo nne za uzalendo zimeimbwa kwa ukamilifu wake kupitia visa na matukio yaliyomo kwenye kitabu. Nyimbo hizi ni Tazama Ramani, Tanzania nakupenda, Mungu Ibariki, Tumejaaliwa sisi Tanzania n.k



Riwaya inatoa elimu ya kina ya kitaalamu juu ya UKIMWI, kuhoji, unyonyeshaji watoto, elimu kwa wapiga kura, ujasiliamali, pamoja na namna ya kuendeleza talanta ama ujuzi. Riwaya inatoa misingi ya kujifunza kwa watu wote wanaosaka maarifa.

Ni Riwaya ya usasa, imetumia fasihi ya majaribio na mwingiliano matini.

Uthibiti wa Ubora wa Kitabu
Riwaya ya Kwaheri imefanyiwa mapitio, maoni na maboresho na wafuatao :-
i. Taasisi
 Taasisi ya Elimu Tanzania; Baraza la Kiswahili la Taifa; pamoja na Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI).

ii. Wataalamu wa Lugha
 Prof. Mugyabuso M. Mulokozi; Dkt. Neema Mturo; Edwin Charles Semzaba (Marehemu); Wanachuo mbalimbali.

5. Hadhira Lengwa
 Hadhira ya kitabu hiki ni jamii nzima. Kutokana na kutumia lugha rahisi.
 Wanafunzi wa viwango mbalimbali vya elimu wataweza kukitumia kitabu
hiki katika somo la Kiswahili hususani fasihi andishi ya Kiswahili.

Ni imani yangu kuwa katika ujenzi wa Taifa letu katika nyanja ya elimu leo kwa kipekee kabisa naweka tofali la KWAHERI katika ujenzi wa ukuta wa nchi yetu ikiwa ni ishara ya muendelezo wa mchango wangu kwa Taifa letu la Tanzania kwa kuunga mkono kwa
vitendo utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Muda mrefu 2011/12 hadi 2024/25, ambapo Serikali imelenga kujenga jamii iliyoelimika na yenye kupenda kujielimisha.

UWARIDI…!!! Karibu Unukie *(Kiitikio)*

10

# ELIZABETH MRAMBA
## Mwandishi wa Punje ya Matumaini

**Na. Mwandishi wetu**

Wengi tunamfahamu kuwa ni mtangazaji wa Televisheni ya Taifa (TBC) tunayemwona mara nyingi akituletea habari na matukio mbalimbali. Ndiyo! Ni kweli kabisa! Hata mimi nilimwona hapo.

Hakuna aliyewahi kujua kuwa mwanadada huyu mwenye umbo la kimiss, ambaye hajaupoteza uzuri aliyotunukiwa na Mungu kuwa ni mwandishi wa vitabu. Hakika wengi walishangaa na kushtuka.

Jicho la UWARIDI lilimwona, na kuutambua mchango wake katika uwanja wa fasihi. Hivyo basi tunu ya Ngao ya Mtunzi ikamhusu. Katika msimu huu wa pili wa tamasha hilo hadhimu, tuzo ya heshima na utambuzi wa mchango wake ikamfikia.

Bi. Elizabeth Mramba. Licha ya kutunukiwa Ngao ya Mtunzi, siku hii alitupatia kitabu kipya cha "CHEMBE YA MATUMAINI" kilihozinduliwa na Waziri Mkuu Mh. Kassim Majaliwa (MB), siku chache kabla ya tukio hili. Katika kitabu hicho, Elizabeth anatuletea mapenzi, usaliti na dawa za kulevya.

Kitabu chake cha Mtumwa Kwenye Nchi Huru mwandishi amenuia kuleta mabadiliko ya fikra. Elizabeth anaeleza kwa kifupi, "Kwenye hicho kitabu  tunamwona mhusikaa anavyopambana, yeye ni mnyonge, hana kitu, hana nguvu, lakini hakati tama, anapambana, ikitokea hiki anapambana. Anapambana na watu wakubwa ambao siyo kitu rahisi (…) Tunasema nchi iko huru lakini watumwa ni wengi. Kama huwezi kuzungumza maana yake huwezi kupata haki yako.

Elizabeth anaeleza kuwa kipaji chake kimechagizwa na mama yake aliyekuwa akimletea vitabu tangu akiwa na umri mdogo, na anaamini vitabu hivyo vilimjenga kufika hapo alipo.

Katika hafla hii, Elizabeth alifuatana na mama yake Bi. Grace Mramba, mumewe na watoto. Anasema kuwa uandishi aliuanza hasa alipokuwa Sekondari.

Ngurumo ya Mwandishi tunampongeza sana kwa Ngao aliyopata na tunamtakia heri na Baraka katika kazi yake ya uandishi wa habari na vitabu.




**ELIZABETH MRAMBA**
**Mwandishi wa Punje ya Matumaini**



# JOSEPH SHALUWA AIPAISHA ‘GLOBAL’ KWA NGAO YA MTUNZI

**Jina la Joseph Shaluwa si geni kwenye masikio ya Watanzania wengi. Anajulikana kwa kipaji chake cha uandishi**



SHIGONGO ampongeza Shaluwa kung’ara Mjue Mtunzi

**wa riwaya zilizojaa kila aina ya burudani.**

Anasema eti hakuamini alivyopewa taarifa kuwa amekuwa mmoja wale watakaotunukiwa Ngao hiyo ya heshima. Ngao ambayo mpaka sasa wametunukiwa waandishi sita tu hapa Tanzania. Ana furaha isiyo kifani kwakuwa anaona ndoto yake aliyoiota siku nyingi inaenda kutimia.

“UWARIDI imenipa heshima kubwa sana kaka”

Hii niyo kauli pekee aliyoniambia.

Licha ya kutunukiwa Ngao hiyo ya heshima Bwana Joseph amezindua kitabu chake kipya kiitwacho

HILIKI YA TUNU, TOTO LA CHUMBAGENI

Jamani, ni balaa humo!

Joseph Shaluwa amestahili kupokea Ngao hiyo kwani ameandika kazi nyingi sana magazetini, za burudani na pia mahusiano.

Mwaka huu 2022 amebarikiwa kutinmiza miaka kumi (10) ya ndoa. Na siku hii ya Elite Mjue Mtunzi alifuatana na familia



yake.

Ni mwandishi na mhariri katika magazeti ya Global Publishers. Kitu pekee alichokionesha kama uungwana kwake ni kumkumbuka Yule aliyemshika mkono katika safari nzima ya uandishi ambaye ni Zugaby Akilimia.





Ngao hii hakuiona yake peke yake, bali ya wote waliomsaidia hapa na pale katika fasihi. Ukipitia ukurasa wake katika Faebook utaona kila aliyemgusa katika maisha yake ya uandishi kamjumlisha katika tuzo hii.

Baada ya hili akajikuta akipewa nafasi ya kuandika bonge la Chombezo katika gazeti pendwa la michezo la Champion ‘CHUMBA CHA SCRUB’. Mwenyewe anakiri kuwa alikuwa akiimezea mate nafasi hiyo yenye donge nono.

Kwa sasa kaenda mbali zaidi, ameanzisha kampuni ya uchapaji wa vitabu, akijaribu kuwasaidia vijana wanaopenda kutimiza ndoto zao katika uandishi.

Hongera sana Joseph Shaluwa… Mwenye Mungu akujalie mema zaidi.



# IBRAHIM MARIJANI GAMA NGAO YA MTUNZI IMEMHUSU

**Na Mwandishi wetu**

**Ni mwandishi kutoka mji wa kihistoria. Mji mdogo wa Bagamoyo unaojulikana kote duniani. Ni mji uliobeba historia kubwa ya nchi hii kabla ya ukoloni.**

Mji huu ndiko anakotokea mwanafasihi huyu, mghani wa mashairi na mwanazuoni aliyebobea kwenye elimu ya dini.

Hana hila hata umtazamapo machoni. Kwa namna moja au nyingine, ni mwenye mkono wa sadaka katika kusaidia waandishi wanaochipukia. Hata mimi mwandishi wa makala hii nimekula sana wali pale nyumbani kwake Bagamoyo.

Yeye ndiye aliyetuandikia riwaya iliyojaa taharuri ya BARUA KUTOKA JELA. Kishapo akatuletea BALAA na kuja kutupoza na HEHEEE KANTANGAZE. CHURA Na 3 ndiyo kitabu chake kipya katika mtindo wa ushairi kilichosheheni beti za kutosha, mishororo isiyokinai kwa vina virefu vyenye mizani iliyolingana.

Siku ya tarehe 3 katika hafla ya Mjue Mtunzi msimu wa pili, chini ya ufadhili wa Elite Bookstore, Ibrahim Marijan Gama alitunukiwa Ngao ya Mtunzi ambayo ni tuzo ya heshima kwa kutambua mchango wake katika fasihi. Ni tuzo pekee Tanzania inayotolewa na Umoja wa Waandishi wa Riwaya wenye Dira UWARIDI.

Mswahili huyu aliyejawa lahaja ya Kiswahili cha Bagamoyo, alijitambulisha kwa kughani ubeti mmoja wa shairi uliowafanya watu waone viti vya moto. Nderemo, vifijo na vigeregere bila kusahau makofi vilimsindikiza.

Inaweza kupendeza zaidi tukimwita *Malenga wa zama zetu*.

Yeye mwenyewe ameandika kwenye ukuta wa akaunti yake ya Facebook.

...Siku ya tarehe 03/07/2022 haitasahaulika katika maisha yangu. UWARIDI wameniheshimisha mno, kwa kuniona natosha kupokea tuzo ya juu kabisa iitwayo MJUE MTUNZI.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia,. Prof Adolf Mkenda, ameweza kunikabidhi tuzo hiyo ya heshima.

Hakika imenitia nguvu, hamasa na ari zaidi katika kuitendea haki fasihi andishi. Nitaendelea kuwapa burudani watanzania na dunia kwa ujumla.

Pia nichukue nafasi hii kuipongeza kamati nzima, ikiwa chini ya rais wa UWARIDI, Hussein Issa Tuwa kwa kuweza kufanya kazi yao kwa weledi na nidhamu kubwa sana.

Shukran za kipekee ziende kwa mpambanaji Maundu Mwingizi (Alwatan Kikoko) panda shuka za ngazi na lifti, nenda rudi za mara kwa mara, zimeweza kulifanikisha jambo kwa ubora mkubwa sana. Mungu akubariki sana.

Kwa kila aliehusika katika jambo hilo kongole nyingi zimemhusu. Silaha yetu ya Umoja na mshikamano, iendelee...



# JE WAMJUA MSOMAJI BORA WA VITABU ALIYETAMBULIWA NA UWARIDI?




**ITOSHE kusema 'anastahili kabisa!'. Wapo watu waliojaza vitabu kwenye mashelfu ndani ya sebule zao, wapo waliojaza kwenye masanduku na wapo wanaonunua kila kitabu ili mradi aonekane kanunua.**

Lakini huyu bwana amejaza vitabu hivyo kichwani mwake. Ni mkazi wa Bagamoyo ambaye ELITE MJUE MTUNZI msimu wa pili imemwona kuwa ni mfano wa wapenda kusoma vitabu. Anaitwa Bwana Peter Chapusa kutoka Bagamoyo mjini.

Katika hafla ya Mjue Mtunzi msimu wa pili, Peter Chapusa alitunukiwa cheti cha heshima cha kumtambua kama msomaji bora wa vitabu. Cheti alichotunukiwa na Mgeni rasmi Waziri wa Elimu Mheshimiwa Adolf Mkenda.

Ngurumo ya Mwandishi hatukumwacha hivi hivi. Na hapa ni mazungumzo yetu.

Ngurumo: Umejisikiaje baada ya kuchaguliwa kuwa msomaji bora wa riwaya?

Chapusa: Kwakweli nimejisikia vizuri sana kwa heshima kubwa niliyopewa.

Ngurumo: Tueleze kwa kifupi historia yako katika muktadha mzima wa usomaji wa vitabu hususan wa riwaya...

Chapusa: Nakumbuka nimeanza kusoma vitabu vya riwaya mwaka 1983 nikiwa darasa la nne. Kitabu changu cha kwanza kilikuwa kinaitwa KABWE MAKANIKA mtunzi ni Mzee Zahir Zorro

Ngurumo: Kitu gani kinakusukuma kutumia pesa nyingi sana kununua vitabu?

Chapusa: Ni mapenzi yangu katika usomaji wa riwaya. Lakini zaidi ni kuwaunga mkono waandishi wa riwaya, wasije kufikiri kuwa kazi zao hazina wasomaji.

Ngurumo: kwa kuwa wewe ni msomaji mahiri wa vitabu; tuambie, kuna tofauti gani kati ya waandishi wa zamani na sasa…

Chapusa: Tofauti siyo kubwa sana kwa sababu visa mikasa ni ileile. Tofauti ipo tu katika upangiliaji.

Ngurumo: Unaweza kutuambia idadi ya vitabu ulivyosoma maishani mwako?

Chapusa: Mpaka sasa namiliki vitabu zaidi ya 400 ambavyo ninavyo na nimevisoma.

Ngurumo: Unawaambia nini wapenzi wa vitabu na unawapa hamasa gani?

Chapusa: jambo la kwanza, tupende kusoma vitabu vya riwaya vinavyoandikwa na waandishi wetu wa nyumbani Tanzania. Jambo la pili tusibague waandishi wa riwaya, la tatu ni jitihada pekee ndiyo humsaidia mtu kufikia malengo yake.

Ngurumo: Umelionaje tamasha la Mjue Mtunzi? Unafikiri litakuwa na athari chanya kwa waandishi na wasomaji?

Chapusa: Tamasha limefana sana, hongera na pongezi kwa waandaaji pamoja na mdhamini Elite Bookstore.

Ushauri wangu kwa sisi wasomaji na watunzi tupendane na tushirikiane. Ninyi waandishi wa riwaya ni wapishi na sisi wasomaji ni walaji. Kuna baadhi ya waandishi wa riwaya vitabu vyao hawapeleki pale Kinondoni, hivyo huwa vigumu kuwafikia baadhi ya wasomaji.

Asante sana!

Licha ya kupewa cheti hicho, Bwana Chapusa alikabidhiwa koba lililosheheni vitabu kutoka Elite Bookstore. Koba alilokabidhiwa na Mheshimiwa waziri.

Furaha iliyoje!






# ELITE MJUE MTUNZI MSIMU WA PILI

## NUKUU YA HOTUBA YA MGENI RASMI

Baadhi ya nukuu kutoka katika hotuba ya Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Adolf Mkenda (MB)

"...Tuanze na UWARIDI. Hawa tayari wapo na wamejipanga. Watafanya kazi zao mkiwasaidia au msipowasaidia..."

“Kilichonifurahisha zaidi kwa kweli ni kuona watu wamekuja na familia(...)Naona watoto wapo humu [ukumbini]. Yaani imekuwa ni kama tamasha kwa kweli. Kuna wake, waume, wazazi. Ni kitu kimoja kizuri na najisikia vizuri sana kukiona.”



“Kikubwa ambacho tumeshafanya, na ambacho tumekiweka kwenye bajeti, tumeamua sasa tutakuwa tunachagua waandishi waliofanya kazi nzuri halafu tutagharamia uchapaji wa vitabu hivyo,”

“Na tunafanya hivyo ili UWARIDI ioneshe kwamba unaweza kuendesha maisha yako kwa kuwa mwandishi tu,”

“Kwa hiyo, kama unaweza kuandika kitu kizuri, halafu kikachapwa bila kuingia gharama yoyote, hiyo inaweza kufanikisha dira hiyo. Kwa hiyo, hilo tumeliweka kwenye bajeti ya Wizara ya Elimu kwa mwaka 2022/2023.”

“Nitoe wito kwa taasisi na makampuni mengine kusaidia pia shughuli hizi za uandishi na uchapishaji,”

“Na pahali pa kuanzia papo. Tuanze na UWARIDI. Hawa tayari wapo na wamejipanga, watafanya kazi zao mkiwasaidia au msipowasaidia. Kuwasaidia ni kusukuma gari moshi ambalo limeanza mwendo tayari.”

Aidha Waziri Mkenda alivishukuru vyombo vya habari vilivyokuwepo hususan Azam TV, SnS na wengineo na kuomba makampuni zaidi kujitokeza kudhamini tukio lijalo.

# MAPICHAPICHA



**Tangazo**

# Elite BOOKSTORE

## Wauzaji na wasambazaji wa vitabu wanaoongoza Tanzania




| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Elite Bookstore | http://www.elitestore.co.tz | +255 658 780 015 | info@elitestore.o.tz | Mbezi Beach, Kariakoo, Nyerere Road & Moshi |







www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

Jarida hili hutolewa na Jamvi la Simulizi kila mwezi
jamvilasimulizi@gmail.com